



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KILIMO

## TAARIFA KWA UMMA

14 Desemba 2024, Dodoma

Wizara ya Kilimo inapenda kuutaarifu Umma kuwa inatarajia kufanya maboresho ya mfumo wake wa kuombea Vibali mbalimbali vya Mazao na Viuatilifu vya Kilimo.

Maboresho hayo yatasaidia kuongeza ufanisi wa mfumo na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wateja wetu, hususan wafanyabiashara.

Zoezi hili linatarajiwa kuanza tarehe **14 Desemba 2024 saa sita (6) usiku** hadi tarehe **15 Desemba 2024 saa sita (6) mchana**.

Kutokana na zoezi hilo, huduma ya mfumo wa kuombea vibali vya **ATMIS** utakosekana kwa muda ulioelezwa hapo juu.

Wizara inaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

*Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.*